

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA RUKWA MHESHIMIWA
ZELOTE STEPHEN ZELOTE ALIYOITOA WAKATI WA KILELE
CHA WIKI YA SHERIA NCHINI KANDA YA SUMBAWANGA
TAREHE 02 FEBRUARI, 2017**

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi, Kanda ya Sumbawanga,
Mheshimiwa Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga.
Mheshimiwa Naibu Msajili mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga,
Mheshimiwa Mtendaji Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga,
Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,
Waheshimiwa Wabunge wote mliopo hapa
Wakili wa Serikali Mfawidhi wa Mkoa wa Rukwa,
Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga,
Mheshimiwa Mstahiki Meya wa Manispaa
Mheshimiwa Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa
Waheshimiwa Viongozi wa Madhehebu ya Dini
Wakurugenzi mliopo hapa,
Waheshimiwa Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Wilaya,
Waheshimiwa Mahakimu ngazi zote na Wasaidizi wa Sheria na majaji,
Mawakili wa Serikali,
Waheshimiwa Mawakili wa kijitegemea,
Mheshimiwa Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya
Sumbawanga,
Viongozi mbalimbali wa Serikali,
Viongozi mbalimbali wa Vyama vya Siasa na asadi za kiraia,
Watumishi wa Mahakama wa Kada mbalimbali,
Ndugu Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Kwanza napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana mahali hapa siku hii ya leo tukiwa salama na wenyewe afya ya kutosha.

Kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Viongozi wa Mahakama Kuu Kanda ya Sumbawanga kwa kunipa heshima ya kuwa "Mgeni rasmi" katika Siku hii adhimu ya kilele cha Wiki ya Sheria Nchini.

"Asanteni sana kwa heshima hii"

Nichukue fursa hii pia kuwapongeza kwa maandalizi mazuri ya shughuli hii ya kuhitimisha Wiki ya Sheria Nchini "**Hongereni sana**"

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Napenda kuchukua nafasi hii kukukaribisha wewe binafsi Mheshimiwa Jaji John S. Mgeta pamoja na Mheshimiwa Jaji wa Mahakama Kuu Dr. Adam J. Mambi Mkoani Rukwa. Nasema hivyo kwa sababu wengi wetu mmetukuta.

Nikushukuru pia Mheshimiwa Jaji Mfawidhi kwa ushirikiano wako wa hali ya juu ambao umeonyesha katika kipindi kifupi tangu umefika baina ya watumishi hata kati ya taasisi zingine na hata mwananchi nmmoja mmoja. Tafadhali endeleva jambo hilo kwani ni malighafi muhimu.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Sitaacha kuipongeza na kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua mbalimbali inayochukua kuboresha huduma za utoaji wa haki katika nchi yetu ikiwa ni pamoja na Mkoa wetu wa Rukwa. Tunapongeza kwa dhati kabisa hatua ya hivi karibuni aliyoichukua Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake kwa kuwapa rasilimali fedha. *Roma haikujengwa kwa siku moja hivyo; tunaamini juhudzi za Serikali ni endelevu katika kuboresha huduma za Mahakama.*

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Niwapongeze pia watumishi wote wa Idara ya Mahakama toka Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama Kuu unayoongoza hapa Rukwa kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuwashudumia wananchi.

Pia nawapongeza marafiki wa kimahakama wakiwemo Mawakili wa Serikali na Mawakili wa kujitegemea, Wazee wa Mabaraza, na wadau wengine ambao kwa njia moja ama nyingine wameshirikiana na Mahakama katika kufanikisha shughuli zake.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kupitia Kauli mbiu ya mwaka huu katika Wiki ya Sheria isemayo “**UMUHIMU WA UTOAJI HAKI KWAWAKATI KUWEZESHA UKUAJI WA UCHUMI**” hii ni kauli mbiu nzito, muhimu na inayoongoza mioyo ya watu wengi na zaidi endapo itaenda sambamba na kutimiza yafuatayo:-

1. Kupambana na vitendo vya Rushwa.
2. Kutokomeza vitendo vya utovu wa Maadili na mgongano wa Kimaslahi.
3. Kujiepusha na mienendo mibaya sehemu za kazi kama vile; kujihusisha na mijadala ya kisiasa mahali pa kazi.
4. Kujiepusha na urasimu na uzembe katika utoaji wa haki.

Waliopo mstari wa mbele kurekebisha haya ni Mahakama yenyewe na uwezo huo mnao. Nimeyasema na ninayasisitiza haya kwa lengo la kuona Mahakama zetu zinajijengea heshima na kuwa na taswira nzuri kwa umma (Public trust).

Katika hili la utoaji haki upo umuhimu wa kuona kamati za Maadili za Mahakama ngazi zote zinafanya kazi kama sheria inavyoagiza. Na ni wajibu wa Mahakama kuimarisha mawasiliano ili kuondoa vikwazo vya mawasiliano kati ya Mahakama na Umma kwa kuzingatia mfumo mzuri ambao tayari mnao.

Kwa upande wa Mawakili wa taasisi zinazohusika na shughuli za Mahakama itoshe kusema kwamba wakae chini na kutafakari sana kauli mbiu hii. Umuhimu wa UTOAJI HAKI KWA WAKATI KUWEZESHA UKUAJI WA UCHUMI. Wasiwe tayari kutumika kutengeneza barabara ya kuchelewesha haki kamwe.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Katika hotuba yako umebainisha mambo mbalimbali yenyе kuhitaji kutazamwa ili kuleta ufanisi zaidi katika mfumo wa Kimahakama. Tukiwa ni Serikali tumeyasikia na tutayachukua ili nasi tuone ni katika maeneo gani tunaweza kutoa mapendekezo ama ushauri kupitia mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Jaji Mfawidhi,

Kauli mbiu ya utoaji haki kwa wakati inaendana kabisa na kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa kazi tu inayosisitiza kila mtu afanye kazi. Kazi mojawapo ni hii ya kwenu ya utoaji wa haki kwa wakati, kupiga vita dhuluma, uonevu, ukwepaji wa kodi, ubadhilifu wa mali ya umma na uzembe. Mahakama pekee ndicho chombo chenye wajibu huo. Fanyeni kazi yenu bila urasimu ama ukiritimba. Mtaheshimika na mtapata thawabu ya Mwenyezi Mungu.

Tunaipongeza serikali kwa kuanzisha Mahakama ya Rushwa na uhujumu uchumi kwa lengo la kupambana na maovu hayo niliyoyaainisha hapo juu.

Baada ya kusema hayo natamka wazi kwamba Maadhimisho ya Wiki ya Sheria Nchini Kanda ya Sumbawanga yamehitimishwa rasmi.

Zelote Stephen Zelote
MKUU WA MKOA RUKWA

